## Ujeuri na mwisho mbaya

Prof. Muhammad Mukhtar Jumaa

Waziri wa Wakfu

**Ujeuri na mwisho mbaya ni mambo mawili yaondayo sambamba wala hayatengani. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema :{ Enyi watu! Jeuri zenu zitakudhuruni wenyewe. Hii ni starehe ya maisha ya dunia tu. Kisha marejeo yenu ni kwetu, na hapo tutakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda.} (Yunus; 23). Na anasema pia {Ama kina A'di walijivuna katika nchi bila ya haki , na wakasema: Nani aliye kuwa na nguvu kushinda sisi ? Kwani wao hawakuona kwamba Mwenyezi Mungu aliye waumba ni Mwenye nguvu kushinda wao? Na wao wakawa wanazikataa Ishara zetu!. 16 Basi tuliwapelekea upepo wa kimbunga katika sikuza ukorofi, ili tuwaonjeshe adhabu ya kuwa hizi katika uhai wa duniani, na bila ya shaka adhabu ya Akhera ina ukali(khezyy) zaidi, na wala wao hawatanusuriwa.} (Fussilat; 15-16). Na anaendelea kusema { Walipo jifakharisha katika waliyo kanywa tuliwaambia: Kuweni manyani wa kudharauliwa } (Al aaraf; 166). Na wasomi wameeleza kuwa Mwenyezi Mungu huunusuru umma ulio na uadilifu hata kama ni wa kikafiri na wala haunusuru umma ulio na dhuluma hata kama ni waumini.**

**Ujeuri unaweza kuwa ni kwa mtu au kwa kundi nalo ni lile liitwalo "kundi la kijeuri" na inaweza pia kuwa ujeuri kwa taifa. Ama kuhusu mtu au kikundi au makundi yatakayofanya ujeuri na kuvuka mipaka ya haki basi mwenyezi Mungu hatowaacha anatashika na kuwapa malipo wanayostahiki, kwani anasema: { Na ndio kama hivyo ndivyo inavyo kuwa Mola wako Mlezi anapo ikamata miji**

**inapo kuwa imedhulumu. Hakika mkamato wake ni mchungu na mkali.} (Hud;102).**

**Na anasema Mwenyezi Mungu kuhusu Qaruni, {Hakika Qaruni alikuwa katika watu wa Musa, lakini aliwafanyia dhulma. Na tulimpa khazina ambazo funguo zake zinawatopeza watu wenye nguvu kuzichukua. Walipo mwambia watu wake: Usijigambe! Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanao jigamba. 77. Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi.Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi. 78. Akasema: Kwa hakika nimepewa haya kwa sababu ya ilimu niliyo nayo. Je! Hakujua kwamba Mwenyezi Mungu kesha waangamiza, katika vizazi vya walio kabla yake, watu walio kuwa wenye nguvu zaidi kuliko yeye,na wenye makundi makubwa zaidi kuliko yake. Na wakosefu hawataulizwa khabari ya dhambi zao. 79. Basi akawatokea watu wake katika pambo lake.Wakasema wale walio kuwa wanataka maisha ya duniani:Laiti tungeli kuwa tunayo kama aliyo pewa Qaruni! Hakika yeye ni mwenye bahati kubwa. 80. Na wakasema wale walio pewa ilimu: Ole wenu!Malipo ya Mwenyezi Mungu ni bora kwa mwenye kuamini naakatenda mema. Wala hawatapewa hayo isipo kuwa wenye subira. 81. Basi tukamdidimiza yeye na nyumba yake katika ardhi; wala halikuwepo kundi lolote la kumnusuru kwa Mwenyezi Mungu, wala hakuwa miongoni mwa wanaojitetea.}(Al qasas; 76-81)**

**Na kuhusu kisa cha nabii Saleh pamoja na watu wake, Mwenyezi Mungu anasema {Na wakamuuwa yule ngamia, na wakaasi amri ya Mola Mlezi wao, na wakasema: Ewe Saleh! Tuletee unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa**

**Mitume. 78. Basi tetemeko la ardhi likawanyakua, na kulipokucha wakawa majumbani mwao kifudifudi wamekwishakufa.} (Alaaraf; 77-79).**

**Ama kuhusu kisa cha nabii Shuib (rehema na amani zimshukie) pamoja na watu wake Mwenyezi Mungu anasema {95. Kama kwamba hawakuwamo humo. Zingatia walivyoangamia watu wa Madyana, kama walivyo angamia watu waThamud!Na ilipo fika amri yetu, tulimwokoa Shua'ibu na wale walio amini pamoja naye kwa rehema yetu. Na ukelele uliwanyakua walio dhulumu, na wakapamba ukiwa majumbani mwao wamekufa kifudifudi!} (Hud; 94-95)**

**Na Mtume wetu (Rehma na amani zimshukie) "Mwenyezi Mungu humpa muda dhalimu mpaka anapoamua kumchukua basi hapo hatowezatoroka." Dhuluma ni kiza siku ya kiyama, na vitimbwi havirudi isipokuwa kwa wenyewe.**

**Hivyo basi, ninasisitiza zaidi kuwa mwisho wa taifa lenye dhuluma ni kutoweka, na amesema kweli mashairi Hafidh Ibrahim aliposema katika ushairi wake mzuri:**

**Misri inajieleza wenyewe.**

**Nchi ngapi zimenifanyia ujeuri**

**Kisha zikatoweka, kwani huo ndio mwisho wake**

**Na hakuna aliyenilenga kisha akawa salama**

**Mwenyezi Mungu amelihifadhi jeshi lake tokea zamani.**

**Nchi itendayo dhuluma na mataifa yaliyojijenga kidhuluma zinajiwekea sababu za kuporomoka na kuanguka kwa haraka sana.**

**Na makundi ambayo yanayofanya utumiaji wa mabavu, dhuluma, ujeuri na kuvuka mipaka katika kutenda maovu kwa mfano wa yale makundi yanayotelekeza mauaji ya kujitolea muhanga na kungamiza, na kurikodi namna wanavyowachinja watu na kuunguza mwili wake. Pamoja na kudhalilisha watu, na kuuza wanawake kama ni mateka wa kivita, kubomoa tamaduni na majengo na kuangamiza kila kilicho na roho na kisicho na roho, hao wanajibebesha sababu za kuanguka kwao na kuangamia, kwani Mwenyezi Mungu hapendi uharibifu wala wenye kufanya uharibifu. Na kwa ajili hiyo mimi ninatoa bishara ya kuwa kuangamia kwa kundi la wapiganaji wa dola la kiisilamu na makundi mengine ya Alqaida na maadui wa nyumba tukufu ya Qudsi, boko haramu na makundi mengineyo ya kikatili - kuangamia – kwao kupo karibuni, {NaMwenyezi Mungu ndiye Mwenye kushinda katika jambo lake, lakini watu wengi hawajui.} (Yusuf; 21)**